JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# Kupima Jitihada za Kuondoa Umasikini

## Fahamu Mfumo wa Ufuatiliaji Umasikini nchini Tanzania

Idara ya Kuondoa Umasikini
Ofisi ya Makamu wa Rais

Agosti 2002

# YALIYOMO

*DIBAJI*

*KWA NINI TUNAHITAJI MFUMO WA NAMNA HII?* 3

Kwa nini tunahitaji mfumo wa ufuatiliaji umasikini?

Nini maana ya mipango inayozingatia taarifa sahihi na kwa nini ni muhimu?

*MUUNDO WA MFUMO HUU UKO VIPI?* 5

Nini kilichomo kwenye Mpango Kamambe wa Ufuatiliaji Umasikini?

Ni kwa jinsi gani Mfumo wa Ufuatiliaji Umasikini unaendeshwa?

Nini maana ya Tathmini Shirikishi ya Umaskini?

*NI JINSI GANI MFUMO HUU UNAWEZA KUTUMIKA?* 8

Je kuna nafasi ya tawala za mikoa na serikali za mitaa kwenye mfumo huu?

Taasisi na jumuiya huru za kiraia zinaweza kuchangia vipi kwenye mfumo huu?

Ni kwa namna gani ninaweza kuingiza taarifa kwenye mfumo huu?

*MFUMO HUU UTAGHARIMU KIASI GANI CHA FEDHA?* 10

Nani anaugharimia mfumo huu?

Watu maskini watanufaika vipi kutokana na mfumo huu?

*NI WAPI NITAPATA TAARIFA ZAIDI KUHUSU JITIHADA ZA KUONDOA UMASIKINI TANZANIA?* 11

Ni wapi ninaweza kupata nakala ya Mpango Kamambe wa Ufuatiliaji Umasikini?

Nini matokeo muhimu ya kazi za Mfumo wa Ufuatiliaji Umasikini?

*VIAMBATANISHO*

Vipengele muhimu vya Mfumo wa Taifa wa Ufuatiliaji Umasikini 14

Muundo wa Kiutawala wa Mfumo wa Ufuatiliaji Umasikini 15

Wajumbe wataalum wa Makundi Manne ya Utendaji wa Kiufundi (TWG) 16

Orodha ya tovuti muhimu 17

Vigezo/viashiria vya kufuatilia umasikini 19

*SHUKRANI*

# DIBAJI

Mkakati wa Kupunguza Umasikini nchini Tanzania (PRSP) ni mkakati wa muda wa kati wa kupunguza umasikini na ni sehemu ya Mpango wa Kuzifutia Madeni Nchi Masikini (HIPC). Mkakati huu unalenga kuifanya Serikali kupunguza matumizi, lakini kuelekeza zaidi nguvu na jitihada zake katika shughuli zinazolenga kupunguza umasikini, na kuchukua hatua nyingine mahususi zisizohusu matumizi ya fedha zinazoweza kusaidia katika jitihada hizi za kupunguza umasikini.

Watu wengi walishiriki katika kuuandaa mkakati huu, na wengi zaidi watashiriki katika kuutekeleza na kuufanya ulete matokeo yaliyokusudiwa. Mpango huu unaorodhesha baadhi ya sababu zinazowafanya watu wawe masikini na kupendekeza njia na hatua kadhaa za kukabiliana nazo. Mkakati wa Kupunguza Umasikini ni tofauti na mipango mingine kwani umeweka malengo yaliyo wazi na bayana na unawataka wananchi washiriki kikamilifu katika utekelezaji wake.

Kuna haja ya haraka ya kujenga uwezo wa watu mbalimbali katika kufuatilia shughuli zilizoanzishwa chini ya Mkakati wa Kuondoa Umasikini. Aidha, wananchi wanahitaji kusaidia katika uchambuzi wa taarifa mbalimbali zinazokusanywa na kubaini taarifa hizo zinamaanisha nini katika sera nzima ya kuondoa umasikini.

Mpango Kamambe wa Kufuatilia Umasikini uliandaliwa hapo mwezi Desemba 2001 ili kuiwezesha Serikali ya Tanzania na wadau wengine kuelewa iwapo mikakati kadhaa ya kuondoa umasikini imekuwa na matokeo yaliyokusudiwa. Mpango huu unabainisha shughuli kadhaa zitakazofanyika katika kipindi cha miaka mitatu ijayo zitakazowezesha kupima kiwango cha umasikini.

Kufuatia kuandaliwa kwa Mpango Kamambe wa Kufuatilia Umasikini, Idara ya Kupunguza Umasikini katika Ofisi ya Makamu wa Rais, imekuwa ikipokea maswali kadhaa kuhusu mfumo wa ufuatiliaji umasikini. Katika jitihada za kujibu maswali hayo, kijitabu hiki cha mwongozo kiliandaliwa. Zaidi ya nakala 20,000 za kijitabu hiki (katika lugha za Kiingereza na Kiswahili) zitasambazwa nchini kote Tanzania.

Tunatarajia kuwa kijitabu hiki kitatoa majibu kwa maswali tunayoulizwa mara kwa mara na kwamba wahusika mbalimbali watakaopenda kupata taarifa zadi wataweza kuwasiliana nasi. Ni wazi kuwa kijitabu hiki si muhtasari wa kina wa mambo yote yaliyomo katika Mpango Kamambe wa Kufuatilia Umasikini. Lengo la kijitabu hiki ni kuwasilisha masuala ya msingi kuhusu namna mfumo huo unavyofanya kazi na hivyo kuibua hamasa ya kutaka taarifa zaidi miongoni mwa watu ambao wangependa kushiriki kwa njia moja ama nyingine katika jitihada za kufuatilia matokeo ya shughuli za kuondoa umasikini nchini.

R. Mollel
Katibu Mkuu

Ofisi ya Makamu wa Rais

Agosti 2002

# UMASIKINI NI NINI NA TUNAWEZA KUUPIMA VIPI?

Siyo rahisi sana kuelezea maana ya umasikini kwa sababu watu mbalimbali wana uelewa tofauti tofauti wa tatizo hili. Uelewa huo unajumuisha masuala mbalimbali kama:

- mtu kutokuwa na uhakika wa kupata chakula chake na matibabu;
- mtu kushindwa kumudu gharama za mavazi na makazi bora;
- mtu kukosa nafasi sawa ya kupata elimu bora na huduma bora za afya, pamoja na  na vitu vingine kama vile maji safi na salama, barabara nzuri na huduma ya kuaminika ya usafiri wa umma;
- mtu kutotendewa haki na wafanyabiashara na viongozi wa ngazi mbalimbali (kijiji, mitaa, kikanda, kitaifa  na kimataifa);
- mtu kutokuwa na sauti katika mambo yanayohusu maisha yake (kwenye eneo lake, kikanda, kitaifa na kimataifa);
- mtu kuwa katika hatari ya kufanywa masikini kutokana na kuwa katika kundi la watu wanaowekwa pembezoni na kunyimwa haki zao (Mathalan, walemavu, yatima, wazazi wasio na waume au wake, wazee na watu wanaoishi na VVU/UKIMWI)

Kwa kuwa kuna njia nyingi tofauti za kuuangalia umasikini, pia kuna njia nyingi za kujaribu kuupunguza. Njia hizi ni pamoja na:

- kutumia vizuri maliasili zetu na vipaji vilivyopo kuzalisha mali, kujipatia kipato na ajira;
- kutilia mkazo na kusaidia maendeleo ya biashara halali zenye kuleta manufaa (biashara ndogo ndogo, za kati na zile kubwa);
- kuhakikisha kuwa watu wana fursa ya kupata huduma bora za kijamii na miundombinu;
- kuandaa mazingira bora ili watu wajisikie wako salama kwenye makazi yao na wanaweza kuziamini mamlaka zilizopo;
- kuweka mipango muafaka na madhubuti ya kuwalinda watu walio kwenye makundi hatari zaidi na yanayoweza kunyimwa haki zao za kimsingi.



### *Kwa nini tunauhitaji mfumo huu?*

Siyo rahisi kupunguza umasikini. Umasikini unawahusisha watu wengi, walio katika ngazi mbalimbali kwenye jamii na ambao wanakabiliwa na matatizo tofauti tofauti katika maeneo mbalimbali. Tunahitaji kufanya kazi kwa pamoja ili tusipoteze muda, nguvu na fedha kwa kutokuwasiliana na kukwamishana. Hii inamaanisha kuwa tunahitaji kujiwekea miundo na taratibu zinazokubalika kwa wote. Hii ina maana kuwa tunahitaji kuwa na MFUMO mahsusi.

Watu wengi tayari wanakusanya taarifa muhimu kuhusiana na umasikini, lakini mara nyingi hawatumii taarifa hizi kwa jinsi inavyotakiwa. Kazi nyingi za ukusanyaji wa taarifa hizo siyo rasmi na haziangalii masuala yaliyopewa kipaumbele kitaifa. Hali kadhalika, mara nyingi hakuna maelewano ya awali baina ya wakusanyaji taarifa hizo na wale wanaotarajiwa kuzitumia. Hii inamaanisha kwamba bado kuna fursa kubwa ya kuboresha namna tunavyokusanya taarifa hizi na namna tunavyozitumia ili tuweze kubuni na kupanga mipango inayotokana na taarifa sahihi.

Hakuna njia moja pekee ya kupima hali ya umasikini inayoweza kushughulikia matatizo na njia mbalimbali za kuyakabili zilizotajwa. Hivyo tutahitaji kutumia njia mbalimbali na kujitahidi kuunganisha matokeo ya njia zote hizo ili tuweze kuweka mipango yetu kwa kuzingatia taarifa sahihi.

Tunahitaji MFUMO wa ufuatiliaji hali ya umasikini ili tuweze kupanga na kukusanya pamoja taarifa kutoka kwenye vyanzo mbalimbali, kuzichambua ili ziweze kutuongoza katika kubuni sera na mipango yetu ya kupunguza umasikini. Nyingi ya sera na mipango hii hutengenezwa katika ngazi ya kitaifa. Hata hivyo, kupitia Mpango wa Mabadiliko wa Serikali za Mitaa mamlaka za mikoa na wilaya zinapewa madaraka na wajibu zaidi wa kubuni sera na mipango yao ya kupunguza umasikini.

Mfumo wa ufuatiliaji umasikini utakusanya taarifa kutoka kwenye vyanzo vikuu vitatu:

- **Taarifa zinazotokana na mfumo za utawala** zitakuwa zikikusanywa na serikali za mitaa, mikoa na idara za serikali kuu (mfano taarifa kuhusu; “idadi ya wanafunzi wanaokatisha masomo ya elimu ya msingi” kutoka mamlaka za elimu; “kiwango cha vifo vya watoto wachanga” kutoka mamlaka za afya na kadhalika);

- **Uchunguzi rasmi** utafanywa na Kitengo cha Takwimu cha Taifa (kwa mfano, Sensa ya Watu na Makazi, Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya, Utafiti juu ya Idadi ya Watu na Afya, Utafiti wa Hali ya Ajira na Nguvu Kazi, na Utafiti kuhusu Hali ya Kilimo);

- Tafiti maalum zitafanywa na watafiti mbalimbali wanaojitegemea. Tafiti hizi zitawahusisha watu wa kawaida badala ya kuwatumia tu kama vyanzo vya taarifa. Matokeo ya tafiti hizi yatasaidia kufafanua sababu zitakazokuwa zinaeleza mabadiliko yatakayokuwa yamejitokeza katika takwimu kutoka katika vyanzo viwili vya mwanzo.

Pamoja na kukusanya taarifa hizi, mfumo wa ufuatiliaji umasikini, utawasaidia na kuwahamasisha watu wa kawaida na viongozi kwenye maeneo yote kuchambua, kutathmini na kuzisambaza taarifa hizi. Pia mfumo huu utawahimiza wahusika wote kutumia taarifa sahihi zitakazokusanywa katika mfumo huu katika kupanga sera na mipango madhubuti na kufanya ufuatiliaji na tathmini nzuri zaidi ya sera na mipango hiyo.

> *Serikali inakusudia kuendelea kuongeza kiwango cha uwakilishi wa watu masikini na wadau wengine katika utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya mkakati wa kupunguza umasikini na hata katika mapitio na kuuboresha mpango huo.*
>
> *Waraka wa Mkakati wa Kupunguza Umasikini (PRSP) Oktoba 2000.*

## *Nini maana ya upangaji unaozingatia taarifa sahihi na kwanini upangaji huo ni muhimu?*

Watu hupanga mipango kwa kuzingatia jinsi wanavyoielewa dunia. Jinsi gani wanavyoielewa dunia, hutegemea nini wanakichofahamu, kwa kuzingatia takwimu au taarifa walizonazo. Ikiwa watu hawafahamu mambo mengi na ikiwa kile wanachokifahamu si sahihi, basi uelewa wao na mipango watakayoipanga kutokana na uelewa huo haitakuwa mizuri.

Ukusanyaji wa taarifa ambao haujaratibiwa na kupangwa vyema, ni bora kuliko kutokukusanya au kutafuta taarifa kabisa. Lakini hali inaweza kuwa bora zaidi iwapo tutakuwa na mfumo uliandaliwa vizuri wa ukusanyaji wa taarifa na ambao unajumuisha taarifa nyingi na za aina nyingi kwa kadri itakavyowezekana. Kwa kuutumia vyema mfumo huo tutaweza kutoa maamuzi bora zaidi, kubuni sera nzuri zaidi na kutumia raslimali zetu vyema zaidi katika kutatua matatizo yanayohitaji utatuzi wa haraka.

Upangaji sera kwa kuzingatia taarifa au takwimu sahihi utaihimiza na kuisaidia serikali na watumiaji wengine wa takwimu au taarifa hizo katika:

- kukusanya na kuchambua taarifa sahihi na baadaye kuchapisha matokeo ya uchambuzi huo na kuyafanyia kazi;
- kuwashawishi watu kuwa taarifa na takwimu halisi na sahihi ni muhimu na ndizo zinazofaa kutumika wakati tunaposhauri kuundwa kwa sera nzuri zaidi katika jamii yetu;
- kuwashawishi waandaaji sera na wanatakwimu kushirikiana kwa karibu zaidi. Ni jambo zuri sana pale waandaaji wa sera wanaposhiriki katika utayarishaji wa mifumo ya ukusanyaji na uchambuzi takwimu na taarifa, hivyo kuzifanya taarifa hizo ziweze kutumika na kuwa na manufaa.

> *Kama sharti la msingi, mtu aliyefanikiwa zaidi maishani ni yule mwenye taarifa nzuri na sahihi.*
>
> Benjamin Disraeli;
> (1804 - 1881)
> Waziri Mkuu wa Uingereza

## MFUMO HUU UMEBUNIWA VIPI?

Wadau wengi walishiriki katika uundaji wa mfumo wa ufuatiliaji umasikini. Kwa hali hiyo tunaweza kuwa na uhakika kwamba takwimu na taarifa mbalimbali zilizo na manufaa zitakusanywa na kuchambuliwa kwa namna inayoratibiwa, na hivyo kwa ufanisi zaidi. Taarifa na ripoti za tafiti mbalimbali zitapatikana kwa urahisi na zitafikishwa kwa watu wa kawaida kwa namna ambayo itawawezesha kuzielewa kwa urahisi.

(Angalia kiambatanisho 1 kwa kuona vipengele muhimu vya Mfumo wa Taifa wa Ufuatiliaji Umasikini)

## *Nini kilichomo kwenye mpango kamambe wa ufuatiliaji umasikini?*

Mpango Kamambe wa Ufuatiliaji Umasikini unaweka wazi kazi zitakazofanyika katika kipindi cha miaka mitatu ijayo. Huu ni mpango unaoendelea kwa sababu kila mwaka unatoa mpango mpya wa miaka mitatu mbele. Kila eneo katika mpango huu limewekewa gharama yake, na gharama hizo kwa ujumla zimeingizwa katika bajeti ya serikali. Mpango huu pia unaelezea hatua za kujenga uwezo wa kila eneo na mfumo kwa ujumla. Hatua hii inalenga katika kuhakikisha kwamba kunakuwa na watendaji wa kutosha wenye ufahamu, maarifa na vifaa vinavyohitajika kwa ajili ya kutekeleza mpango huu. Kwa maana hiyo, mfumo huu utawasaidia wadau wote kupanga sera na mipango na kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa kuzingatia taarifa na takwimu sahihi walizopatiwa.

## *Mfumo wa ufuatiliaji umasikini unaendeshwa vipi?*

Katika warsha ya wadau iliyofanyika hapo Oktoba mwaka 2000, washiriki walikubaliana kuundwa kwa kamati ya kitaifa ya uendeshaji na usimamizi wa ufuatiliaji umasikini, ikiwa na wawakilishi kutoka kila eneo muhimu la serikali, taasisi na jumuiya huru za raia, wanataaluma na sekta binafsi. Aidha, warsha hiyo ilipendekeza kuundwa kwa **makundi manne ya utendaji wa kiufundi (TWG).** Makundi haya tayari yameshaundwa.

(Angalia kiambatanisho cha pili, chenye kielelezo kinachoonyesha jinsi mfumo huu unavyofanya kazi).

Kamati ya Uendeshaji wa Ufuatiliaji Umasikini iliundwa Mei mwaka 2001. Mwenyekiti wa kamati hii ni Katibu Mkuu katika Ofisi ya Makamu wa Rais. Kamati ina wajumbe kutoka sehemu mbalimbali ikiwa ni pamoja na taasisi za kitaaluma, taasisi na jumuiya huru za raia, vikundi vya kidini, mashirika ya maendeleo ya kimataifa, wizara muhimu zilizomo kwenye PRSP, na sekta binafsi.

Kazi kuu ya kamati hii ni kusimamia zoezi zima la ufuatiliaji umasikini na kutoa miongozo, kupitia taarifa za utekelezaji na kupitisha mipango ya kazi za makundi ya utendaji wa kiufundi. Vilevile kamati ina jukumu la kutafuta fedha ili kuwezesha utekelezaji wa mfumo mzima wa ufuatiliaji umasikini kwa vitendo. Aidha, kamati hii inasimamia utayarishaji wa ripoti ya kila mwaka kuhusu hali ya umasikini nchini Tanzania.

Kamati ya kiufundi ya Mkakati wa Kupunguza Umasikini (PRS) ipo chini ya uenyekiti wa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha. Kamati hii inajumuisha wawakilishi kutoka makundi manne ya kiufundi. Kazi yake kuu ni kuratibu na kuboresha mawazo ya makundi ya kiufundi, kabla hayajawasilishwa katika kamati ya uendeshaji.

Sekretarieti ya ufuatiliaji umasikini ina wajumbe kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, Wizara ya Fedha, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji. Sekretarieti hii inafanya kazi sio tu kwa Kamati ya Uendeshaji Ufuatiliaji Umasikini na Kamati ya Kiufundi ya Mkakati wa Kupunguza Umasikini, bali pia kwa Kamati ya Mawaziri.

Kazi za sekretarieti hii ni pamoja na kuandaa mikutano ya kamati inazozihudumia; kuyataarifu makundi ya utendaji wa kiufundi kuhusu maamuzi yaliyofikiwa na kamati hizo; kuandaa nyaraka za kamati mbalimbali; na kuratibu uandaaji wa nyaraka mbalimbali kwa ajili ya kamati zote. Sekretarieti hii pia ina jukumu la kuratibu mashauriano baina ya wadau kuhusu Mkakati wa Kupunguza Umasikini, na kuandaa ripoti ya mwaka juu ya hali ya umasikini nchini Tanzania.

Makundi manne **ya utendaji wa kiufundi** ni haya yafuatayo:

- ***Kundi linalohusika na utafutaji takwimu au taarifa na sensa***
  Kundi hili linaongozwa na Kitengo cha Taifa cha Takwimu. Kundi hili Imeandaa mpango wa kutafuta taarifa na takwimu mbalimbali utakaoondelea hadi mwaka 2012. Mpango huu wa kazi utahusisha shughuli za Sensa ya Taifa ya watu na makazi, Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya, Utafiti juu ya Idadi ya Watu na Afya, Utafiti wa Hali ya Ajira na Nguvu Kazi, na Utafiti kuhusu Hali ya Kilimo.

- ***Kundi linalohusika na ukusanyaji takwimu zinazotokana wa mfumo wa utawala***
  Kundi hili lipo chini ya uenyekiti wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kundi hili lina jukumu la kuboresha mfumo wa serikali kuu, serikali za mikoa na za mitaa kuchambua, kubadilishana na kusambaza taarifa mbalimbali. Mifumo iliyoboreshwa itawasaidia watu wengi zaidi kupata taarifa muhimu na zenye manufaa, kwa urahisi zaidi.

- ***Kundi linalohusika na utafiti na uchambuzi***
  Kundi hili linaongozwa na Ofisi ya Rais - Mipango na Ubinafsishaji. Kundi hili ndilo linaloamua kuhusu maeneo ya kupewa kipaumbele na kupendekeza njia za upatikanaji fedha kwa ajili ya utafiti na uchambuzi. Aidha, kundi hili linatoa uchambuzi na kuijulisha jamii kuhusu viwango na vyanzo vya umasikini nchini na matokeo ya sera mbalimbali za kupunguza umasikini. Mbinu tofauti za utafiti na ukusanyaji taarifa zitatumika, hata hivyo mkazo zaidi unawekwa katika mbinu za tathmini shirikishi za umasikini (PPA) ambazo ndizo zinazo bainisha wazi jinsi watu masikini wanavyoelewa hali zao.

- ***Kundi linalohusika na usambazaji, uhamasishaji na kujenga mwamko***
  Kundi hili linaongozwa na Ofisi ya Makamu wa Rais. Hili ndilo linaloratibu programu ya kusambaza taarifa zinazopatikana kupitia mfumo mzima wa ufuatiliaji umasikini. Aidha, linawahamasisha na kuwafahamisha wadau mbalimbali kuhusu hali ya umasikini na hatua mbalimbali zinazofikiwa katika kukabiliana nao. Pamoja na masuala mengine, kundi hili limeazimia na kujizatiti kuwafikishia wananchi katika ngazi ya chini kabisa, taarifa mbalimbali kwa njia ambayo itakuwa rahisi kwao kuzielewa na kuzitumia ili waweze kuchukua hatua mwafaka za kukabiliana na umasikini katika na maeneo au mazingira yao.

Makundi haya ya utendaji wa kiufundi yanaratibu na kutoa mwongozo wa kazi zinazofanyika katika maeneo mbalimbali, na si kufanya kazi hizo yenyewe . Ni wazi kuwa kama makundi haya yatakuwa makubwa mno itakuwa ni vigumu kuyaendesha vyema. Kwa mantiki hiyo, makundi haya yameundwa na idadi ndogo ya wajumbe, ambayo hata hivyo inazingatia uwakilishi wenye uwiano ukiwajumuisha pia wanaharakati mahiri katika masuala ya jinsia na mazingira.

Hii inamaanisha kwamba, iwapo taasisi au jumuiya huru ya kiraia ina mawazo fulani ya kuchangia katika kamati hizi, inaweza kufanya hivyo kwa kupitia mwakilishi wa katika kundi husika la kiufundi. Iwapo wewe unaona kuwa unastahili kujiunga na moja ya makundi haya, unaweza kuwasiliana mwenyekiti wa kundi husika kwa kupitia Sekretarieti ya Ufuatiliaji Umasikini.

Maelezo zaidi kuhusu uanachama wa makundi haya manne yanapatikana kwenye kiambatanisho cha tatu (3).

### *Nini maana ya tathmini shirikishi ya umasikini?*

Takwimu nyingi zinazokusanywa katika Mfumo wa Ufuatiliaji Umasikini zimeegemea zaidi kwenye kubainisha matokeo yanayoweza kuhesabika au yale yanayoonekana kwa macho. Takwimu hizi zinaweza kutueleza mengi kuhusu mambo yanayofanyika lakini si sababu za kufanyika kwa mambo hayo. Waathirika wenyewe wa tatizo la umasikini ndio watakaoweza kujibu vyema zaidi maswali kuhusu sababu za wao kufanya mambo kwa namna fulani na si vinginevyo. Wao ndio wenye kujua vyema zaidi hisia walizonazo na namna wanavyoielewa hali ya maisha waliyonayo. Taarifa kama hizi zinapokusanywa ndizo zinazoweza kuelezea sababu za msingi zisizoweza kupimika kwa namba au kuonekana kwa macho za hali halisi iliyopo.

Tathmini shirikishi za umasikini zinatoa fursa kwa watu masikini na wale waishio katika mazingira magumu zaidi kueleza wanakifikiria nini kuhusu umasikini. Vile vile wanaweza kutoa mawazo yao kuhusu sababu za mabadiliko yanayotokea katika maisha na mazingira yao.

Watafiti wanaofanya tathmini shirikishi za umasikini hujaribu zaidi kuzungumza na mtu mmoja mmoja badala kuzungumza na kundi kubwa la watu au taasasi. Mchakato wa jumla wa tathmini shirikishi ya umasikini umejengeka katika kuwashirikisha na kuwawezesha watu masikini na wale walio katika makundi yanayoishi katika mazingira magumu kueleza iwapo sera na mipango mbalimbali ya kuondoa umasikini imeleta au imeshindwa kuleta mabadiliko katika maisha yao.



## NI JINSI GANI MFUMO HUU UNAWEZA KUTUMIKA?

Mfumo wa Ufuatiliaji Umasikini ni tofauti na mifumo iliyokuwa ikitumika hapo awali kwa sababu:

- watumiaji wa taarifa na takwimu zitakazopatikana wameshirikishwa katika kuamua ni taarifa zipi zitafutwe na kukusanywa;

- hivi sasa watayarishaji sera, wapangaji mipango na wafadhili kwenye ngazi zote wanaelewa vyema zaidi umuhimu wa kutumia taarifa au takwimu sahihi katika kutayarisha sera na mipango ya kuondoa umasikini;

- kundi la utendaji wa kiufundi la uhamasishaji, uhimizaji na usambazaji limeundwa kuhakikisha kuwa taarifa na takwimu zinapatikana kwa wingi na kwa urahisi kwa kadri itakavyowezekana kwa wadau wote na njia itakayowawezesha kuzielewa taarifa na takwimu hizo kwa urahisi;

- wakati wote mfumo wa ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa unafuatiliwa kwa makini na kufanyiwa mapitio na wadau mbalimbali ili kama kutakuwa na haja ya kuufanyia mabadiliko, basi mabadiliko hayo yaweze kufanyika haraka.

Mfumo wa Ufuatiliaji Umasikini umebuniwa ili ujumuishe wadau wengi kadri iwezekanavyo. Katika harakati inayoendelea dhidi ya umasikini, mfumo huu utawasaidia wale wote watakaoutumia kutumia vyema zaidi muda, rasilimali na juhudi zao. Watu wanaweza kuutumia mfumo huu katika njia kuu mbili: - wanaweza kuchangia na kuingiza taarifa ndani ya mfumo, na pia wanaweza kutoa taarifa kutoka kwenye mfumo huu.


### *Je kuna nafasi ya tawala za mikoa na serikali za mitaa katika mfumo huu?*

Watumishi katika tawala za mikoa na serikali za mitaa watashirikishwa kwa karibu katika Mfumo wa Ufatiliaji Umasikini kwa njia zifuatazo:

- kusaidia kutafuta na kuchambua taarifa zilizokusanywa katika ngazi za vitongoji, mitaa mikoa hadi taifa;

- kutumia taarifa zilizokusanywa katika kutayarisha sera, kupanga, kufuatilia na kutathmini shughuli za kupunguza umasikini katika ngazi ya kitongoji/mtaa na kwenye ngazi ya wilaya;

- kuhakikisha matokeo ya ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa yanawafikia watu kwa urahisi na kwa kiwango kikubwa na kuwahimiza kuzijadili na kuzitumia taarifa hizo.



Watumishi wa ofisi za tawala za mikoa na serikali za mitaa watakuwa ni watendaji muhimu sana katika kazi za kundi la utendaji wa kiufundi linaloshughulikia ukusanyaji wa takwimu na taarifa kutoka katika na mfumo wa utawala. Makundi mengine ya utendaji wa kiufundi yanahitaji taarifa hizi ili kutoka katika mfumo wa utawala ili kukamilisha ukusanyaji wa taarifa, hasa ikizingatiwa ukubwa wa nchi na muda ambao ungehitajika kukusanya taarifa hizo zote. Taarifa zinazopatikana katika eneo fulani zinaweza kutumika katika eneo husika, lakini pia waandaji sera katika ngazi ya kitaifa, wanazihitaji taarifa hizo ili kulinganisha mahitaji tofauti ya watu tofauti katika maeneo tofauti nchini.

Vilevile Mfumo wa Ufuatiliaji Umasikini utafanya kazi kwa karibu na Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Serikali za Mitaa. Kuanzishwa kwa mfumo huu ni sehemu ya Programu ya Mabadiliko katika Serikali za Mitaa. Mifumo hii miwili inajumuisha kuwapatia watendaji hao vifaa na mafunzo. Hii itasaidia sana kuwawezesha wafanyakazi wa mamlaka za wilaya na tawala za mikoa nchini na kuwa na ufanisi zaidi katika ukusanyaji, utunzaji, uchambuzi na utumiaji wa takwimu zinazokusanya katika mfumo wa kawaida utawala na utendaji wa serikali.

### *Taasisi, vikundi na jumuiya huru za raia zinaweza kuchangia vipi katika mfumo huu?*

Taasisi za hiari na jumuiya huru za kiraia zimeshirikishwa katika hatua zote za utayarishaji wa Mfumo wa Ufuatiliaji Umasikini na zina wawakilishi katika Kamati ya Uendeshaji Ufuatiliaji Umasikini na hali kadhalika katika makundi ya utendaji wa kiufundi .

Taasisi na jumuiya huru za kiraia zitakuwa muhimu zaidi katika kutekeleza Tathmini Shirikishi ya Umasikini itakayoendeshwa na kusimamiwa na Kundi la Utafiti na Uchambuzi na katika kazi ya kuwafikia wananchi itakayoendeshwa na Kundi la Usambazaji, Uhamasishaji na Uhimizaji.

Mfumo wa Ufuatiliaji Umasikini unajaribu kuwahusisha wadau wengi kwa kadri iwezekanavyo. Hata hivyo ufuatiliaji wa kujitegemea unaofanywa na taasisi, vikundi na jumuiya huru za kiraia nao pia unathaminiwa. Mfumo huu kwa ujumla wake, unaweza kusaidi na upo tayari kuhimiza kufanywa kwa uchunguzi wa kujitegemea na kisha kuyaingiza matokeo ya uchunguzi huo katika hazina yake na kusaidia kuyasambaza.

Kundi la utendaji wa kiufundi linaloshughulikia Utafiti na Uchambuzi hutayarisha na kupitia mara kwa mara programu ya kubainisha maeneo ya utafiti yanayostahili kupewa kipaumbele. Kiasi fulani cha fedha kimetengwa kwa ajili ya kusaidia kazi za ufuatiliaji umasikini zinazofanywa na taasisi na jumuiya huru za kiraia. Fedha hizi zinatolewa pale ambapo kazi hizo zinaangukia katika maeneo yaliyopewa kipaumbele na kundi hili la utafiti na uchambuzi.

ZINGATIA: Fedha za Mfumo wa Ufuatiliaji Umasikini zinaweza kutumika tu kusaidia miradi ya kupambana na umasikini inayolenga katika shughuli za utafiti.

### *Ni jinsi gani ninaweza kuingiza taarifa mbalimbali katika mfumo wa ufuatiliaji umasikini?*

Kwa njia isiyo rasmi, ufuatiliaji umasikini hufanyika kila wakati. Watu wote, wawe masikini au matajiri, wazee au vijana, wanaoishi mijini au vijijini, watu binafsi au



makundi, huchukua hatua mbalimbali kulingana na taarifa na ushahidi walionao. Mfumo wa Ufuatiliaji Umasikini utawasaidia watu wa aina mbalimbali kupata taarifa na ushahidi wanaouhitaji ili kufanya maamuzi mazuri na yenye manufaa faida. Kadri taarifa nyingi zinavyopatikana kupitia mfumo huu, ndivyo mfumo wenyewe unavyozidi kuimarika na kuwa na ufanisi.

Tanzania inahitaji taarifa na ushahidi unaoonyesha jinsi hali ya umasikini inavyobadilika na kuweka bayana iwapo juhudi za serikali za kupunguza umasikini zimekuwa na mafanikio ama la. Mfumo huu umebuniwa ili kuwawezesha wadau wote wanaoshiriki katika zoezi hili kutumia vizuri zaidi muda, juhudi na rasilimali zao.

Mfumo wa Ufuatiliaji Umasikini unakaribisha na kupokea taarifa na ushahidi uliopatikana kutokana na tafiti au uchunguzi wa kujitegemea unaofanywa na watu binafsi au taasisi mbalimbali. Iwapo utakuwa na ushahidi au taarifa yoyote ambayo ungependa iingizwe katika Mfumo wa Ufuatiliaji Umasikini, tafadhali itume kwa Sekretarieti ya Ufuatiliaji Umasikini katika Ofisi ya Makamu wa Rais. Sekretarieti nayo itapeleka taarifa hizo kwenye kundi husika la utendaji wa kiufundi.

## MFUMO WA UFUATILIAJI UMASIKINI UNAGHARIMU KIASI GANI?

Mfumo wa Ufuatiliaji Umasikini utagharimu takriban shilingi za Kitanzania bilioni 2.5 kwa mwaka. Kiasi hiki cha fedha kinaweza kuonekana kuwa ni kikubwa, lakini ni kiasi cha asilimia 0.6 tu ya kiasi cha shilingi za Kitanzania bilioni 516 zilizotengwa kwa ajili ya bajeti ya Mkakati mzima wa Kupunguza Umasikini kwa mwaka 2002/03.

Iwapo Mfumo wa Ufuatiliaji Umasikini usingekuwepo, basi ukusanyaji wa taarifa na takwimu mbalimbali usingeweza kupangwa na kuratibiwa vyema. Kwa hali hiyo, muda, jitihada na fedha nyingi zingepotea bure. Mfumo huu mpya ulioandaliwa kwa makini unamaanisha kuwa tutawza kiasi kikubwa cha fedha na kupata thamani halisi ya fedha zitakazotumika.

Bajeti yenye mchanganuo wa kina wa mahitaji ya fedha kwa kila kundi kati ya makundi manne ya utendaji wa kiufundi na kwa ajili ya utawala wa mfumo mzima imeshaandaliwa. Maelezo zaidi kuhusu suala hili yanapatikana katika Waraka wa Mpango Kamambe wa Ufuatiliaji Umasikini.

### *Nani anaugharamia mfumo huu?*

Serikali imetoa umuhimu wa kipekee kwa shughuli za kufuatilia umasikini kama sehemu muhimu ya utekelezaji wa shughuli zake. Hivyo imetenga kiasi cha shilingi za Kitanzania bilioni 1.1 katika bajeti yake ya mwaka 2002/2003 kwa ajili ya mfumo. Kiasi kilichobaki cha shilingi bilioni 1.4 kitachangiwa na washirika wake wa maendeleo.

### *Watu masikini watanufaika vipi kutokana na mfumo huu?*

Wananchi hawatanufaika moja kwa moja kutokana na fedha zinazotumiwa chini ya mfumo huu, bali watanufaika sana kutokana na kuboreshwa kwa taratibu za utayarishaji sera, mipango, ufuatiliaji na tathmini zinazozingatia taarifa na takwimu halisi na sahihi katika ngazi ya maeneo wanayoishi, mkoa na taifa.

Pamoja na mambo mengine, mfumo huu utawapa fursa wananchi kufahamu sera sera mbalimbali zinazogusa maisha yao na kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili kuchochea maendeleo yao. Hivyo basi, iwapo mambo yatakwenda kinyume na mipango na ratiba ya utekelezaji wa mipango hiyo, wananchi watakuwa katika nafasi nzuri zaidi ya kuhoji.

> *Tunahitaji msaada kutoka nje ili kutusaidia kuchambua na kuielewa hali na uzoefu wetu vizuri zaidi, lakini sio kutuambia nini tufanye.*
>
> *Harakati ya Bhoomi Sena*
> *(India)*
> *1977*

## NI WAPI NITAPATA TAARIFA ZAIDI JUU YA JITIHADA ZA KUPUNGUZA UMASIKINI NCHINI TANZANIA?

Mfumo wa Ufuatiliaji Umasikini umeundwa kwa namna inayorahisisha upatikanaji wa taarifa. Katika michache ijayo taarifa mbalimbali zitachapishwa. Taarifa hizi zitapatikana katika vijitabu vidogo vidogo na ripoti ambazo utaweza kuzipata katika ofisi za serikali katika wilaya au mkoa wako. Unaweza pia kupata nakala zako mwenyewe kutoka kwa Sekretarieti ya Ufuatiliaji Umasikini (anuani ya sekretarieti hiyo inaonyeshwa nyuma ya jalada la kijitabu hiki). Aidha, nyingi ya taarifa au ripoti zitakazotolewa zitapatikana pia katika tovuti kadha katika mtandao wa mawasiliano ya kompyuta (angalia orodha ya tovuti muhimu katika kiambatanisho cha 5) .

Ni vyema ifahamike kuwa taarifa nyingi zitapatikana pia kupitia magazeti, radio na televisheni na wakati mwingine kupitia mabango na kazi mbalimbali za wasanii wa sanaa za maonyesho. Tafadhali fuatilia kwa karibu ni nini kinachotokea katika eneo unamoishi, wilayani na mkoani kwako, na hata katika ngazi ya kitaifa na uwe tayari kushiriki kikamilifu katika matukio hayo.

Pia unaweza kuorodhesha jina lako na anuani yako katika orodha ya watu na taasisi zinazopelekewa taarifa mbalimbali ili uweze kutumiwa taarifa kuhusu ripoti mbalimbali pindi zitakapokuwa zimeandaliwa. Iwapo ungependa taarifa zaidi tuandikie kwa anuani iliyopo nyuma ya kijitabu hiki.



## *Nitapata wapi nakala ya Mpango Kamambe wa Ufuatiliaji Umasikini?*

Unaweza kupata fursa ya kusoma nakala za Mpango kamambe wa Ufuatiliaji Umasikini kwenye ofisi za serikali katika ngazi ya wilaya na mkoa. Majalada ya nakala hizo yana rangi nyekundu iliyokolea.

Ukihitaji kupata nakala yako mwenyewe, wasiliana na Sekretarieti ya Ufuatiliaji Umasikini kwa anuani iliyoonyeshwa nyuma ya kijitabu hiki.

Kama umeunganishwa katika mtndao wa mawasiliano ya kompyuta unaweza kupata nakala ya bure ya mpango huo kwa kufungua faili lililo katika anuani ifuatayo:
http://www.tzonline.org/pdf/povertymonitoringmasterplan.pdf



## *Mfumo wa kitaifa wa ufuatiliaji umasikini utakuwa na matokeo gani muhimu?*

Kama matokeo ya shughuli za mfumo huu unaweza kutarajia kuchapishwa na kupatikana kwa ripoti zifuatazo:

1. **Ripoti ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya ya 2000/2001**
   Ripoti hii itatoa matokeo ya takwimu kuhusu mabadiliko yanayoweza kuonekana dhahiri (quantitative) zilizokusanywa katika Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya na kuyalinganisha na matokeo ya utafiti kama huo uliofanyika mwaka 1990/1991.

2. **Ripoti ya Hali ya Umasikini na Maendeleo ya Binadamu.**
   Ripoti hii itatoa picha ya maendeleo yaliyofikiwa katika utekelezaji wa malengo ya Mkakati wa Kuondoa Umasikini. Aidha, ripoti hii itaonyesha mambo muhimu yatakayojitokeza katika utafiti na uchambuzi. Mambo haya yataelezea na kufafanua sababu zilizosababisha mabadiliko yatakayojitokeza katika taarifa na takwimu zitakazokusanywa.

3. **Utafiti kuhusu Hali ya Nguvu Kazi Nchini**
   Taarifa hii ya utafiti itabainisha mambo muhimu yatakayojitokeza kuhusu hali ya nguvu kazi nchini Tanzania na itajumuisha kipengele cha ajira mbaya kwa watoto.

4. **Tathmini Shirikishi za Umasikini**
   Tathmini hizi zitatoa picha ya matatizo halisi na hali ngumu za maisha zinazowakabili wananchi.

5. **Mfumo wa Utunzaji Taarifa za Kijamii na Uchumi**
   Huu ni mfumo unaotumia kompyuta ambao ni chanzo kikuu cha taarifa za kitakwimu unaoendeshwa na Kitengo cha Takwimu cha Taifa. Wadau wote wanahimizwa kuutumia mfumo huu.

6. **Taarifa kwa waandaaji sera**:
   Hizi ni ripoti maalumu zinazotumia taarifa au ushahidi kutoka katika mfumo wa ufuatiliaji kuchambua na kufanya mapitio ya masuala fulani mahsusi.

## Vipengele muhimu vya Mfumo wa Taifa wa Ufuatiliaji Umasikini

### Ufafanuzi kuhusu mahitaji ya taarifa:

Wadau wamekubaliana juu ya viashiria muhimu vitakavyotumika katika mfumo huu pamoja na vipaumbele kwa ajili ya ukusanyaji taarifa mbalimbali kuelezea sababu za hali itakayokuwa imejitokeza na hivyo kufanya takwimu kujitosheleza zaidi.

### Mfumo wa kitaasisi:

Kamati ya uendeshaji ya kitaifa ya mfumo wa ufuatiliaji umasikini na makundi manne ya utendaji wa kiufundi yameundwa ili kusimamia na kutekeleza kazi ya mfumo. Muundo mzima wa mfumo huu unajionyesha kwenye kiambatanisho 2.

### Nyenzo za ukusanyaji taarifa au takwimu:

Kuna makundi mawili ya nyenzo za ukusanyaji taarifa na takwimu. Kundi la utendaji wa kiufundi linaloshughulikia utafutaji taarifa au takwimu na sensa linasimamia programu ya miaka kadhaa ya ukusanyaji takwimu mbalimbali itakayotekelezwa na Kitengo cha Takwimu cha Taifa. Kundi la utendaji wa kiufundi linaloshughulikia ukusanyaji takwimu kutoka katika mfumo wa kawaida wa utawala serikalini linasaidia kuweka mipango ya kuboresha na kuinua uwezo wa idara za serikali kuu na serikali za mitaa wa kuchambua na kutumia taarifa zinazokusanywa kila siku katika idara hizo.

### Vipaumbele vya utafiti:

Maswali ya kitafiti yatawasaidia watafiti kukusanya aina ya taarifa ambazo haziwezi kukusanywa katika ukusanyaji wa takwimu na sensa, au katika utendaji wa siku hadi siku katika utawala wa serikali. Taarifa hizi ndizo zitakazo kidhi haja ya kuelezea kwa undani vyanzo na sababu za hali itakayojitokeza na masuala yanayohusu tathmini. Kundi la utendaji wa kiufundi linaloshughulikia utafiti na uchambuzi limeandaa mpango unaoweka utaratibu wa kufuatwa katika utafiti, uchambuzi na tathmini shirikishi za umasikini.

### Mpango wa usambazaji:

Kundi la utendaji wa kiufundi linaloshughulikia usambazaji, uhimizaji na uhamasishaji limetayarisha orodha ya watu watakaotumia takwimu na taarifa zitakazokusanywa na mfumo wa ufuatiliaji umasikini. Pia limefikiria njia nzuri zaidi za kuwawezesha watu hao kupata taarifa na takwimu hizo. Miongoni mwa njia muhimu zitakazotumika katika kusambaza taarifa hizo ni ile ya kupitia Mfumo wa Utunzaji Takwimu Kuhusu Hali ya Kiuchumi na Kijamii nchini Tanzania, (Tanzania Socio-Economic Database) pamoja na tovuti rasmi katika mtandao wa mawasiliano ya kompyuta yenye habari kuhusu Tanzania (Tanzania Online).

### Kujenga uwezo:

Mipango imeandaliwa ili kuhakikisha kuwa wadau wote muhimu wanaoshiriki kwenye mfumo mzima wa ufuatiliaji umasikini wanapata mafunzo na vifaa wanavyohitaji ili waweze kufanya kazi hii kwa tija na ufanisi.

### Gharama:


Bajeti za kina kwa kila kipengele cha Mfumo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji Umasikini na kujumuishwa katika bajeti kuu ya miaka mitatu.

### Taratibu za kuchangia gharama:

Sehemu ya gharama za mfumo huu italipiwa na serikali na sehemu nyingine italipiwa na wabia wa maendeleo.

# KIAMBATANISHO 2

***Muundo mzima wa mfumo wa taifa wa ufuatiliaji umasikini***



# KIAMBATANISHO 3

## *Wajumbe katika makundi ya utendaji wa kiufundi*

### *Kundi linalohusika na utafutaji takwimu na sensa*

*Mwenyekiti:* Mkurugenzi Mkuu wa Kitengo cha Taifa cha Takwimu

*Wajumbe:*
- Benki Kuu ya Tanzania
- Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (DFID)
- Taasisi ya Mafunzo ya Takwimu ya Afrika Mashariki
- Shirika la Kazi la Kimataifa (ILO)
- Shirika la Misaada la Japan (JICA)
- Kitengo cha Taifa cha Takwimu
- Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji
- Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi na Usanifu Majengo (UCLAS)
- Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP)
- Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA)
- Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuwahudumia Watoto (UNICEF)
- Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
- Mpango wa Chakula Duniani (WFP)

### *Kundi linalohusika na ukusanyaji takwimu zinazotokana wa mfumo wa utawala*

*Mwenyekiti:* Mkurugenzi wa Tawala za Mikoa, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

*Wajumbe:*
- Taasisi ya Mafunzo ya Takwimu ya Afrika Mashariki
- Shirika la Misaada la Ireland (Irish Aid)
- Mpango wa Kuboresha Serikali za Mitaa
- Wizara ya Kilimo na Chakula
- Wizara ya Elimu na Utamaduni
- Wizara ya Afya
- Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
- Wizara ya Maji na Mifugo
- Wizara ya Ujenzi
- Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
- Shirika la Maendeleo la Uswisi (SDC)
- Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP)
- Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuwahudumia Watoto (UNICEF)

### *Kundi linalohusika na utafiti na uchambuzi*

*Mwenyekiti:* Mkurgenzi wa Uchumi Mkuu (Macroeconomy), Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji

*Wajumbe:*
- Benki Kuu ya Tanzania
- Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (DFID)
- Taasisi ya Utafiti wa Kiuchumi na Kijamii (ESRF)
- Shirika la Misaada la Japan (JICA)
- Kitengo cha Taifa cha Takwimu
- Ubalozi wa Uholanzi
- Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji
- Kitengo cha Kuondoa Umasikini, Ofisi ya Makamu wa Rais
- Taasisi ya Utafiti wa Kuondoa Umasikini (REPOA)
- Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP)
- Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuwahudumia Watoto (UNICEF)
- Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
- Benki ya Dunia

### *Kundi linalohusika na usambazaji, uhamasishaji na kujenga mwamko*

*Mwenyekiti:* Mkurugenzi wa Kitengo cha Kuondoa Umasikini, Ofisi ya Makamu wa Rais

*Wajumbe:*
- Shirika la CARE International
- Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (DFID)
- HakiKazi Catalyst
- HealthScope
- International Data Vision
- Shirika la Misaada la Ireland (Irish Aid)
- Shirika la Misaada la Japan (JICA)
- Mpango wa Kuboresha Serikali za Mitaa
- Wizara ya Elimu na Utamaduni
- Wizara ya Fedha
- Wizara ya Afya
- Kitengo cha Taifa cha Takwimu
- Baraza la Mazingira la Taifa
- Kitengo cha Kuondoa Umasikini, Ofisi ya Makamu wa Rais
- Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji
- Save the Children
- Mtandao wa Jinsia Tanzania
- Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)
- Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP)
- Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuwahudumia Watoto (UNICEF)
- WaterAid

# KIAMBATANISHO 4

***Tovuti katika mtandao wa mawasiliano ya kompyuta zenye taarifa mbalimbali kuhusu umasikini nchini Tanzania ni pamoja na hizi zifuatazo:***

**Tanzania Online**
www.tzonline.org
*Tovuti hii ina nyaraka nyingi muhimu kuhusu maendeleo na inaonyesha anuani za tovuti nyingine mbalimbali zenye habari nyingi kuhusu maendeleo.*

**Maelezo ya CIA kuhusu Tanzania**
www.cia.gov/cia/publications/factbook/geos/tz.html

**ESRF**
www.esrftz.org
*Taasisi ya Utafiti wa Hali ya Uchumi na Kijamii (ESRF) ni Taasisi isiyo ya Kiserikali inayojihusisha na utafiti unaolenga katika kujenga uwezo wa kufanya uchambuzi wa masuala ya uchumi na yale ya kijamii …*

**Taarifa kuhusu Tanzania katika tovuti ya Benki ya Dunia**
www.worldbank.org/hipc/country-cases/tanzania/tanzania.html
*Benki ya Dunia hutoa mikopo na ushauri kwa zaidi ya nchi 100 zinazoendelea. Benki hii inajulikana pia kama Benki ya Kimataifa ya Ufufuaji Uchumi na maendeleo. Sera, matokeo, uchumi ...*

**Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP)**
www.tgnp.co.tz
*Mtandao huu unafanya kazi zake ukilenga katika kuleta usawa wa kijinsia; mageuzi ya kijamii na kuinua uwezo wa wanawake kushiriki kikamilifu na kuwa na usemi katika mambo yanayogusa maisha yao, kijamii, kisiasa na kiuchumi. Tovuti ya mtandao huu inajumuisha habari na taarifa mbalimbali ikiwa ni pamoja a shughuli zinazofanywa na mtandao huo kwa sasa, programu za elimu, machapisho, taarifa kuhusu ufadhili na anuani ya mtandao wenyewe.*

**Hakikazi Catalyst**
www.hakikazi.org
*Taasisi hii inalenga katika kuchangia mawazo kuhusu namna ya kuinua haki za watu wote kushiriki kikamilifu katika masuala ya kijamii, kiufundi ...*

**Shirikisho la Vyama Visivyo vya Kiserikali Tanzania (TANGO)**
www.tango.or.tz
*Tovuti hii ni mpya! Inajumuisha taarifa nyingi kuhusu taasisi na jumuiya huru za kiraia ikiwa ni pamoja na orodha ya mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) programu mbalimbali za shirikisho hilo, machapisho n.k ...*

**Taarifa kuhusu Tanzania katika tovuti ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF)**
www.imf.org/external/country/tza/index.htm
*Tovuti ya IMF inaonyesha anuani ya tovuti nyingi zenye taarifa muhimu mbalimbali, taarifa kuhusu IMF, Viwango vya fedha zinazotolewa/riba na machapisho ya IMF. Tovuti hiyo inajuisha pia taarifa mpya, viwango na kanuni mbalimbali za shirika hilo, taarifa kuhusu nchi mbalimbali na makala maalumu. Shirika hili linalenga katika kukuza kiwango cha ukuaji wa uchumi kwa kupitia ushirikiano wa kimataifa katika masuala ya fedha na utoaji wa mikopo na misaada ya fedha.*

**REPOA**
www.repoa.or.tz
*Hii ni taasisi isiyo ya Kiserikali inayojihusisha na shughuli na ajenda za utafiti na kutoa taarifa na habari mbalimbali kusaidia utayarishaji wa sera.*

**Tathmini Shirikishi za Umasikini nchini (PPA) Tanzania**
www.esrftz.org/ppa/
*Tovuti hii ina kalenda ya mikutano na matukio mbalimbali kuhusu umasikini. Taasisi ya Utafiti wa Hali ya Uchumi na Kijamii (ESRF) ni Taasisi isiyo ya Kiserikali inayojihusisha na utafiti unaolenga katika kujenga uwezo wa kufanya uchambuzi wa masuala ya uchumi na yale ya kijamii ...*

***Zifuatazo ni baadhi ya nyaraka na ripoti muhimu ambazo tayari zimeshatolewa:***

- **Dira ya Maendeleo ya Tanzania hadi Mwaka 2025**
  www.tzonline.org/pdf/theTanzaniadevelopmentvision.pdf

- **Waraka wa Mkakati wa Taifa wa Kupunguza Umasikini(NPES)**
  www.tanzania.go.tz/poverty.html

- **Mkakati wa Kuisaidia Tanzania (TAS)**
  www.tzdar.or.tz/Harmonisation/TAS.doc

- **Waraka wa Mkakati wa Kupunguza Umasikini (PRSP)**
  www.tzonline.org/pdf/FinalPRSP25.pdf

- **Tanzania bila umasikini**
  www.hakikazi.org/eng

- **Ripoti ya Maendeleo ya Utekelezaji wa Mkakati wa Kupunguza Umasikini kwa mwaka 2000/01**
  www.tzonline.org/pdf/prspprogress01.pdf

- **Mpango kamambe wa ufuatiliaji umasikini**
  www.tzonline.org/pdf/povertymonitoringmasterplan.pdf

- **Ripoti ya kwanza ya Maendeleo ya Tanzania bila Umasikini**
  www.hakikazi.org/eng2

# KIAMBATANISHO 5

## *Viashiria vya ufuatiliaji umasikini*

### *Umasikini wa kipato*
Uwiano katika mahitaji muhimu ya binadamu na umasikini
Uwiano katika mahitaji muhimu maeneo ya mijini na umasikini
Uwiano wa chakula na umasikini
Umiliki mali, pato na umasikini
Kundi la nguvu kazi ambalo sasa halina kazi za kuzalisha
Ukuaji wa pato la ndani la jumla kwa mwaka
Ukuaji wa pato la jumla la ndani katika sekta ya kilimo kwa mwaka
Kiwango cha asilimia cha matengenezo ya barabara na hali nzuri ya barabara inayohitajika

### *Uwezo wa binadamu*
Uwiano wa mtoto wa kike na wa kiume kupata elimu ya msingi
Uwiano wa mtoto wa kike na kiume katika kupata elimu ya sekondari
Kiwango cha umri kutoka elimu ya msingi hadi sekondari
Kiwango cha kuelimika miongoni mwa watu wenye umri wa miaka 15+
Kiwango cha uandikishaji wanafunzi katika elimu ya msingi
Kiwango cha watoto walioacha au walioshindwa kuendelea na elimu ya msingi
Asilimia ya idadi ya wanafunzi waliofaulu darasa la saba katika ngazi A,B,C
Kiwango cha ARI kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano
Kiwango cha ugonjwa wa kuhara kwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano
Idadi ya watu wenye uwezo wa kupata huduma ya maji safi

### *Kuishi*
Idadi ya vifo vya watoto wachanga
Idadi ya vifo vya watoto walio na umri chini ya miaka 5
Kiwango cha kuishi kwa miaka
Kiwango cha seropositive kwa akina mama wenye ujauzito
Wilaya zilizomo kwenye kampeni madhubuti dhidi ya kuleta ufahamu wa ugonjwa wa ukimwi HIV/AIDS
Vifo vya watoto vinavyotokana na ujauzito
Matukio ya ugonjwa wa malaria kali kwa watoto walio na umri chini ya miaka 5
Kiwango cha watoto wenye umri wa chini ya miaka miwili waliopata chanjo zote dhidi ya surua na DPT
Idadi ya watoto waliozalishwa na muuguzi wa afya mwenye utaalamu

### *Ustawi wa jamii (utawala bora)*
Idadi ya mahakama za mwanzo zilizopokea kesi na kuzitolea hukumu
Kiwango cha wastani cha kusuluhisha mizozo ya kibiashara

### *Lishe*
Kimo cha mtoto katika umri ulio chini ya miaka 5
Uzito wa mtoto aliye chini ya umri wa miaka 5
Uzito uliozidi wa mtoto aliye na umri wa chini ya miaka 5

### *Hali ya makundi yaliyo hatarini*
Idadi ya watoto yatima miongoni mwa watoto waliopo
Idadi ya watoto wanaoongoza familia zao
Idadi ya watoto walio katika ajira
Idadi ya watoto walio katika ajira na ambao hawaendi shule
Idadi ya wazee wanaoishi nyumbani ambako hakuna hata mtu katika kaya mwenye uwezo kiuchumi

### *Mazingira muafaka ya maendeleo kiuchumi*
Uwiano wa akiba ya ndani kwa mwezi

> Binadamu kwa upande wao ni lazima wajilazimishe japo kwa muda mfupi kuweka kando mawazo na fikra zao na kuanza kujizoeza kuzingatia ukweli na taarifa zinazoweza kuthibitika
>
> Francis Bacon
> (1561-1626)
> Mwanasayansi wa Uingereza

# SHUKRANI

Kitengo cha Kuondoa Umasikini cha Ofisi ya Makamu wa Rais kinapenda kutoa shukrani kwa watu wafuatao kutokana na mchango wao katika kukitayarisha na kukisambaza kijitabu hiki:

- Wajumbe wa makundi yote ya utendaji wa kiufundi, hususan kundi la usambazaji, uhamasishaji na kujenga mwamko.
- Arthur Van Diesen na Christopher Mushi wa UNDP
- Alana Albee na Kaushi Shah wa DFID
- Esther Obdam wa UNICEF
- Wafanyakazi wa Kitengo cha Kuondoa Umasikini, hususan Anna Mwasha, Paschal Assey na Servus Sagday.
- George Clark wa Caledonia Centre for Social Development
- Emmanuel Kallonga wa Hakikazi Catalyst
- Nisha Sanghvi wa Acex Systems Ltd
- Masood Kipanya
- ColorPrint Tanzania Ltd
- Waheeda Samji na Julia Sampson wa Carpe Diem Ink
- Wengine wote ambao wameshiriki kwa njia moja au nyingine katika uchapishaji wa kijitabu hiki

**Dk. S. Likwelile**

Mwenyekiti

Kundi la Utendaji wa Kiufundi la Usambazaji, Uhamasishaji na Kujenga Mwamko



**Kwa Maelezo Zaidi**
**Tafadhali Wasiliana na**

Sekretarieti ya Ufuatiliaji Umasikini
Idara ya Kuondoa Umasikini
Ghorofa ya 2, Jengo la Maktaba
S.L.P. 5380
Dar-es-Salaam